HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA TOLEO LA 002 | JUNI 2024 | HALIUZWI

# CHUNYA

## ZAWADI YETU

Jarida la Mtandaoni





MHARIRI MKUU
TAMIM H. KAMBONA
Mkurugenzi Mtendaji wilaya ya Chunya

MHARIRI MSAIDIZI
JOSHUA. A. SENGO
Kaimu Mkuu wa kitengo cha Habari Wilaya ya Chunya
FATUMA MTWEVE
Afisa Habari-Wilaya ya Chunya

WAPIGA PICHA
JOSHUA A. SENGO
FATUMA MTWEVE
FRANK T. LYIMO

MSANIFU WA JARIDA
FRANK T. LYIMO
Afisa Habari-Wilaya ya Chunya

# UONGOZI WA WILAYA YA CHUNYA




Mhe. Mbarak Alhaji Batenga
Mkuu wa wilaya ya Chunya



Mhe. Bosco Mwanginde
Mwenyekiti H/Shauri ya Chunya



Mhe. Masache Njelu Kasaka
Mbunge Jimbo la Lupa



Ndugu; Anakleth Michombero
Katibu tawala wilaya ya Chunya



Ndugu; Tamim Kambona
Mkurugenzi Mtendaji - Chunya



# RC HOMER; MKIKAMATA MTU ANATOROSHA TUMBAKU, TAIFISHENI HIYO TUMBAKU

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Mhe Juma Zuberi Homera amewataka wakulima wa zao la Tumbaku Mkoa wa kitumbaku Chunya kutotorosha Tumbaku kwani watakaobainika kutorosha au kuweka uchafu kwenye Tumbaku watachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani sambamba na kutaifisha Tumbaku zilizokamatwa.

Kauli hiyo ilitolewa tarehe 17/05/2024 wakati wa ufunguzi wa soko la ununuzi wa Tumbaku kwenye mkoa wa Kitumbaku Chunya uliofanyika kwenye Chama cha Msingi cha Ushirika cha Kalangali kilichopo kata ya Mtanila ambapo Mkuu wa Mkoa wa Mbeya alikuwa Mgeni rasmi katika hafla ya ufunguzi

“Niwaombe vyombo vya ulinzi na usalama mtu anayeweka mawe kwenye Tumbaku, Mnyimeni dhamana, ni uhujumu uchumi. Hatuwezi tukaharibi taswira ya mkoa wa Mbeya kwa kuweka mawe kwenye Tumbaku, Mkimkamata huyo mtu hakuna kumuonea huruma” Mhe Homera

Homera pia amemuagiza Mkuu wa wilaya ya Chunya kutaifisha Tumbaku itakayokamatwa ikitoroshwa kutoka Chama kimoja kwenda Chama Kingine au ikitoroshwa kwenda nje ya Mkoa wa Kitumbaku Chunya jambo ambalo halikubaliki kulingana na miongozo ya kilimo cha zao la Tumbaku

“Anaye torosha Tumbaku kupeleka kwenye chama kingine mkimkamata Mhe. Mkuu wa wilaya beba hiyo tumbaku inarudi kwenye chama alichotoka itaifishwe asilimia 70 wapate wenyewe kwenye chama na

asilimia 30 iende Halmashauri" Homera

Aidha Mhe Homera amewataka wananchi kuhakikisha hawachanganyi tumbaku na vitu vingine kwani kufanya hivyo ni kujiharibia wao wenyewe, kitu ambacho kitapelekea makampuni kuondoka na kuacha kununua Tumbaku, huku akiwaonya viongozi wa Vyama vya Msingi kuhakikisha Tumbaku haichanganywi na mawe kwani chama kitakachobainika kuruhusu wakulima wake Kuchanganya mawe chama hicho kitafutiwa usajili.

"Niwambieni chama ambacho kitapokea Tumbaku ya namna hiyo hicho chama tutakifuta, wanachama mtaenda kwenye vyama vingine, lazima na chama cha msingi muwe makini, huwezi mkaruhusu tumbaku iwekwe mawe" alisema Mhe. Homera

Kwa upande wa mkuu wa wilaya ya Chunya Mhe Mbarak Alhaji Batenga ametoa rai kwa wakulima wa zao la Tumbaku kuendelea kuhifadhi mazingira na kuhakikisha wanapanda miti ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira unaoambatana na kilimo cha zao la Tumbaku "Zao hili la Tumbaku tumekuwa tukiendeleza kama takwimu ambavyo zinasema, yapo mambo ya msingi wakati tunazalisha na yenyewe tuyazingatie, Mhe Mkuu wa mkoa nimejipa jukumu la kusimamia swala la mazingira ili lisilete changamoto katika biashara yetu hii ya dhahabu ya kijani" Mhe Batenga

Hafla ya ufunguzi wa Msimu wa masoko ya Tumbaku katika mkoa wa kitumbaku Chunya ilifanyika mwishoni mwa juma (Mei 17, 2024) katika ghala la AMCOS ya kijiji cha Kalangali kata ya mtanila wilayani Chunya ambapo Mkuu wa Mkoa wa Mbeya alikuwa Mgeni rasmi katika Hafla hiyo.





# DC BATENGA; "HATUTAKI KUMWACHA MTOTO YEYOTE NYUMA WOTE WAKASOME BILA KUJALI CHANGAMOTO ZAO"




Mkuu wa wilaya ya Chunya Mhe Mbarak Alhaji Batenga ameonya wananchi wa wilaya ya Chunya kuwaficha watoto wenye mahitaji maalumu jambo linalopelekea watoto hao kukosa huduma na haki zao za msingi anazostahili kuzipata ikiwepo haki ya kupata Elimu, haki ya kupendwa na haki ya kupatiwa mahitaji yote muhimu kama watoto wengine

Alitoa onyo hilo tarehe 18/6/2024 katika viwanja vya ofisi ya kata ya Ifumbo wakati akizungumza na wananchi wa kata hiyo katika kuadhimisha siku ya mtoto wa Afrika ambayo huadhimishwa kila tarehe 16 Juni ya kila mwaka lakini Halmashauri ya wilaya ya Chunya wameadhimisha siku hiyo tarehe 18/6/2024

"Kuna watu wanaficha watoto wenye mahitaji maalumu, wanawanyima watoto hao kupata haki yao ya kupata elimu, Serikali imetoa fedha ya kujenga shule mbalimbali kwaajili ya watoto wenye mahitaji maalumu, Chunya tunazo Shule ya Msingi Kibaoni, na shule ya Msingi Makonglosi hivyo wapelekeni watoto shule wapate Elimu. Tunaposherehekea siku ya mtoto wa Afrika hatutaki kumwacha mtoto yeyote nyuma, watoto wote wakasome bila kujali changamoto alizonazo" Alisema Mhe Batenga

Aidha Mhe Batenga aliwataka viongozi wa dini wilayani Chunya kutumia majukwaa yao kuwaongoza waumini kuhakikisha wanapinga ukatili kwa watoto kwani viongozi hao wa dini wanayo nafasi kubwa na muhimu kuhakikisha ukatili unatokomezwa wilayani Chunya na kwakufanya

hivyo watakuwa wametimiza lengo la kuwa na dini mbalimbali katika maeneo yao

"Viongozi wa dini ni



wapeleka ujumbe wazuri sana kwa jamii yetu, hivyo niwaombe viongozi wa dini kufikisha ujumbe kwa watu tunaowaongoza wa kukemea vitendo vya ukatili kwa watoto na hiyo ndiyo ibada sahihi kwa miongozo ya dini zetu" Aliongeza Mhe Batenga

Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii wilaya ya Chunya Bi Twijisye Ephraim aliwataka wananchi wa Ifumbo kutumia maadhimisho hayo kuunganisha nguvu pamoja ili kukemea na kupinga ukatili wanaofanyiwa watoto katika mazingira yao na kwakufanya hivyo watakuwa wanalinda Taifa la kesho

"Lengo la maadhimisho haya kufanyika kila mwaka ni sisi wananchi kujitathimini kwa pamoja na kuunganisha nguvu kwa pamoja ili Tutafute suluhu ya changamoto wanazokumbana nazo watoto bila kujali mtoto huyu ni wako au si wako au mtoto huyu analelewa na nani kwani watoto wote ni watoto wa Taifa zima la Tanzania na ni watoto wetu sote kama jamii" alisema Bi Twijisye

Akitoa salamu za wananchi wa kata ya Ifumbo Mbele y Mkuu wa wilaya ya Chunya Diwani wa kata ya Ifumbo Mh. Weston S. Mpyila aliwataka wananchi wa Ifumb kutowafanyisha kazi kupita kiasi watoto lakini amewataka kuongeza upendo kwa watoto wao ili kuwasaidia kufikia ndoto zao

"Niwasihi wananchi wenzangu tusiwafanyishe kazi wototo wetu kupita kiasi, lakini pia niwaombe kuanzia leo watoto wetu tuwapende na tuwapeleke shule watoto na hili siwaombi maana ni suala la lazima na ndio maana Serikali inajenga miundombinu mbalimbali ya Shule ili watoto wapate elimu, wananchi naomba yote yanayozungumzwa hapa tuyafanyie kazi"Alimesema Mhe Mpyila

Maadhimisho ya siku ya mtoto wa Afrika huadhimishwa kila tarehe 16 Juni ya Kila mwaka yakiwa na lengo la kufanya tathimini na kuchukua hatua katika kuhakikisha watoto wanapata haki zao za msingi bila vizuizi vyovyote. Kwa mwaka huu maadhimisho hayo yaliongozwa na kauli mbiu "Elimu jumuishi kwa watoto, Izingatie Maarifa, Maadili na Stadi za kazi"





# SERIKALI KUPITIA OFISI YA RAIS TAMISEMI IMEJIPANGA KURUDISHA HADHI YA WALIMU NCHINI

Mkurugenzi msaidizi Elimu anayesimamia elimu ya awali na Msingi Kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Mwalimu Suzana Nussu amesema Serikali ya Rais Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan imedhamilia kurudisha hadhi, heshima na thamani ya walimu nchini Tanzania Jambo ambalo litapelekea kufanya kazi kwa kujituma na kwa kujiamini wawapo katika kutekeleza majukumu yao.
Alitoa kauli tarehe 31/5/2024 wakati akizungumza kwenye ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya (Sapanjo) mbele ya walimu kutoka Idara ya elimu awali na msingi pamoja na walimu kutoka idara ya Elimu Sekondari wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake baada ya kuhitimisha ziara kama hiyo Mkoa wa Songwe.
"Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) tunataka hadhi, heshima na haki ya Mwalimu irudi. Hatuwezi kutekeleza hayo kwa kukaa ofisini hivyo ofisi nzima imegawanyika Nchi nzima kuongea na walimu kuhusu hilo lakini pia kutoa mrejesho wa mambo mbalimbali ambayo yanaendelea kutekelezwa na Serikali ya Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan ili kurudisha hadhi ya mwalimu. Mhe Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amesema tuwambie anawapenda sana" alisema Mwalimu Nussu
Aidha, Mwalimu Nussu amewathibitishia walimu wa wilaya ya Chunya kwamba kuanzia Mwezi Januari walimu wameendelea kulipwa madai yao huku akisema zaidi ya walimu 100 (104 walimu kutoka idara ya Elimu ya awali na Msingi, walimu 15 kutoka Idara ya Elimu Sekondari) wilaya hii ya Chunya watapandishwa madaraja kwa

mseleleko kwenda Daraja wanalostahili baada ya takwimu kuonesha wanalipwa mishara ambayo sio ya daraja analostahili kuwepo
Naye Afisa kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI Mwalimu Liliani Nyinge amewakum-

Rais, Tawala za mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwakuipangia walimu wengi wilaya hiyo, tofauti na utaratibu wa kupanga watumishi uliokuwa unatumiwa hapo awali, Hivyo ameomba matumizi ya mfumo huo maalu-



busha walimu waliohudhuria kikao hicho kwamba wanapotekeleza majukumu yao wakumbuke kuzingatia uwezo wa mtoto mmoja mmoja kwanza, utayari wa mtoto huyo kujifunza, umri wake, pamoja na mazingira anayotoka. Mambo hayo manne kwa pamoja yakizingatiwa yanaweza kusaidia kuamua njia sahihi ya kuwasaidia wanafunzi hao na wakapata matokeo sahihi hatimaye kuwa msaada kwa familia zao hapo baadaye.
Awali akitoa taarifa ya Elimu katika Halmashauri ya wilaya ya Chunya, Afisa Elimu awali na Msingi Mwalimu Ferd Y. Mhanze amesema, Halmashauri ya wilaya ya Chunya imenufaika sana na Ofisi ya

mu wa kuwapangia walimu vituo vya kazi uendelee ili Wilaya ya Chunya iendelee kunufaika zaidi na hatimaye lengo la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kuwahudumia wananchi wake kwa kuwapatia Elimu bora litimie Chunya.
"Tunawashukuru TAMISEMI kwa kutumia mfumo maalumu kugawa walimu, kwani wilaya ya Chunya tumepata walimu wengi tofauti na ilivyokuwa hapo awali hivyo ni maombi yetu matumizi ya Mfumo huo wa kuwapanga walimu uendelee ili wilaya ya Chunya tuendelee kupata walimu wengi zaidi na kwakuwa tunashukuru na kushukuru ni namna nyingine ya kuomba hivyo tunaomba muendelee kuitazama Chunya kama mnavyoitazama sasa" Amesema Mwalimu Mhanze
Afisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya Mwalimu Hamis M. Mapato kwa niaba ya Mkurugenzi mtendaji wilaya ya Chunya amesema Halmashauri ya wilaya ya Chunya inafanikiwa kutekeleza vigezo vyote vya upimaji kutokana na ushirikiano mzuri pamoja na uwajibikaji wa walimu kutoka idara zote za Elimu Msingi na Sekondari.
"Mafanikio yaliyosomwa hapa katika taarifa ya Idara za Elimu ya awali na Msingi na Taarifa ya Idara ya Elimu Sekondari yamechagizwa na walimu hawa walioko mbele yako, Tumepita kwenye vituo vyao kuwahimiza kulingana na Vigezo vya upimaji wa ufaulu (Key Perfomrmance indicators KPI). Ndugu washiriki wa kikao hiki tunao ugeni wa Kitaifa umekuja kushuhudia namna tulivyo tekeleza vigezo vya KPI naomba kuwasihi na kuwaomba tusikilize na tumfuatile ili tupate lengo la Serikali kwetu" Amesema Mwalim Mapoto.
Kikao hicho kimehusisha walimu zaidi ya mia tatu na hamsini kutoka idara ya elimu ya awali na msingi, pamoja na idara ya elimu ya Sekondari wilaya ya Chunya, walimu wakuu, wakuu wa shule maafisa Elimu kata na watumishi wa idara za Elimu awali na msingi, idara za elimu sekondari, Idara ya Utumishi, Tume ya utumishi wa walimu (TSC) Ofisi ya Mdhibiti ubora sambamba na ugeni kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI

# UTEKELEZAJI WA ILANI YA CHAMA CHUNYA TUKO VIZURI



Mkuu wa Wilaya ya Chunya Mhe. Mbarak Alhaji Batenga alimwambia Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Mbeya kuwa utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Wilaya ya Chunya unakwenda vizuri huku akitaja baadhi ya maeneo kama ujenzi na usimazi mzuri wa miradi ya maendeleo, ukusanyaji wa mapato ya Serikali pamoja na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi.

Kauli hiyo aliitoa Aprili 6, 2024 wakati akitoa salamu za Serikali mbele ya Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Mbeya wakati wa kilele cha maadhimisho ya wiki ya Umoja wa wazazi wa jumuiya ya Chama Cha Mapinduzi yaliyoadhimishwa kimkoa katika kata ya Sangambi, Halmashauri ya wilaya ya Chunya.

"Nikuhakikishie Mwenyekiti utekelezaji wa Ilani ya chama kwa Wilaya ya Chunya tuko vizuri sana hapa walikuwa wanazungumza juu ya kituo cha afya cha Sangambi naomba nikuhakikishie kwamba kituo hiki tunakijenga kwa kutumia mapato ya ndani lakini pia kwa upande wa ukusanyaji wa mapato ya serikali kwasasa hivi Wilaya ya Chunya ndio tunaongoza kwa ukusanyaji wa mapoato kwa Mkoa wa Mbeya hii ni kutokana na jinsi ambavyo tumejipanga kuitekeleza Ilani" alisema Mhe.Batenga

Akizungumza na hadhara iliyokusanyika katika sherehe hizo Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Mbeya ndugu Patrick Mwalunenge aliyekuwa Mgeni rasmi katika maadhimisho



hayo ameitaka jamii kuwalea watoto katika maadili mazuri ili wawe waadilifu katika maisha yao ya baadaye huku akionya malezi mabaya yanayotolewa na wazazi na walezi kwa watoto wao.

"Leo niwaambie wanasangambi tatizo la mmomonyoko wa maadili ni kubwa sana tumeona kila siku Rais wetu Dkt Samia Suluhu Hassan akitumia gharama kubwa sana kuwabadilisha viongozi katika nafasi zao kutokana na ubadhilifu na udanganyifu katika mali za umma hayo yote yanatoka kwetu sisi kutokana na malezi kwasababu wale ni watoto ambao tumewalea sisi wenyenyewe". Alisema Mwalunenge.

Naye Mwenyekiti wa jumuiya ya wazazi wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Mbeya ndugu James Mwampondele alisema kuwa lengo la maadhimisho hayo kama Jumuiya ya wazazi ni kuhakikisha wanasimamia maadili, malezi , mazingira pamoja na mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ukatili wa Kijinsia kwa kutoa elimu kwa wanajamii na wana CCM ili kutengeneza jamii bora.

Maadhimisho hayo yaliadhimishwa Aprili 6, yakiongozwa na kauli mbiu isemayo Ushindi wa CCM 2024-2025 Umoja wa Wazazi Tupo mstari wa Mbele. Maadhimisho hayo yalienda sambamba na utoaji wa elimu mbalimbali kuhusu mmomonyoko wa maadili kutoka kwa wadau na taasisi mbalimbali, na yamehudhuriwa na viongozi wa chama cha Mapinduzi kuanzia ngazi ya Mkoa hadi ngazi ya jijiji, wanachama wa Chama cha Mapinduzi pamoja na viongozi wa Serikali kutoka ngazi Mbalimbali za uongozi.



# DC BATENGA: "WEKENI VIZURI KUMBUKUMBU ZA UMILIKI WA MAENEO AMBAPO MIRADI INATEKELEZWA"

Mkuu wa wilaya ya Chunya Mhe Mbarak Alhaji Batenga amewataka viongozi wa vijiji na kata kuhakikisha wanaweka vizuri Nyaraka za kumbukumbu za umiliki wa maeneo ambapo miradi mbalimbali ya Maendeleo inajengwa ili kuepuka migogoro ya ardhi mbele pindi kizazi hiki kitakapokuwa kimepita Ametoa kauli hiyo leo tarehe 28/05/2024 wakati akiongoza kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya ya Chunya wakiambata na wataalamu kutoka taasisi mbalimbali za Serikali katika wilaya ya Chunya ili kukagua utekelezaji wa mradi wa maji unaojengwa na shirika la Catholic Relief Services (CRS) kwa gharama ya shilingi milioni mia tatu hamsini na tano Akitoa Taarifa ya utekelezaji wa mradi huo mbele ya Kamati ya Ulinzi na Usalama, Meneja wa mradi huo kutoka Shirika na CRS Bi Bertha Mkepela amesema utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia themanini huku akisema mwishoni mwa mwezi juni mradi huo utakuwa umekamilika

Diwani wa kata ya Kasanga Mhe Mh. Benson B. Msomba amewashukuru wadau kutoka shirika la CRS kwa namna ambavyo wanatekeleza ujenzi wa mradi wa maji katika kata ya Kasanga kwani kupitia mradi huo utapunguza uhitaji wa Maji kwenye kata ya Kasanga maana Kijiji cha Soweto kikipata maji maana yake uhitaji wa maji utabaki kwenye kijiji cha Mawelo "Shukrani kubwa ni kwa Ziara yako wewe Mkuu wa wilaya ya Chunya na Uongozi ulio

ongozana nao pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuweza kutubarikia mradi huu katika kijiji cha Soweto. Mradi huu utapunguza changamoto ya maji kwenye kijiji cha Soweto na najua baada ya kutatua hili kijiji cha Mawelo kitafuata. Mhe Mkuu wa wilaya tupelekee salamu zetu kwa Mhe Rais kwamba Wananchi wa Kata ya Kasanga wanakushukuru sana kumtua Mama Ndoo Kichwani". Amesema Mhe Msomba



Kamati ya Ulinzi na usalama wakiambatana na viongozi kutoka Taasisi Mbalimbali wameanza rasmi ziara ya siku tatu kukagua miradi ya maji inayotekelezwa wilayani Chunya. Ziara hii kwa siku ya kwanza imehusisha kata ya Matundasi, Kata ya Kasanga na kata ya Chalangwa na ziara hiyo itaendelea tena kesho tarehe 29/05/2024 kuendelea kukagua utekelezaji wa Miradi ya maji wilayani Chunya



## Afisa Elimu Mkoa wa Mbeya Awafunda walimu

Afisa elimu Mkoa wa Mbeya Mwalimu Kiduma Mageni amewafunda walimu wa Shule za Msingi na awali wilayani Chunya kwa kuwambia lazima wayapende mazingira yao ya kazi kwani muda mwingi wa Maisha yao hutumia kuwepo mazingira ya Shule na kwakuyapenda Mazingira hayo itavutia walimu kufundisha lakini itavutia wanafunzi kusoma kwa bidii

"Hakikisheni pale shuleni ni sehemu ya kuishi hivyo mazingira yawe yenye kuvutia na pia ongezeni ubunifu katika kufanya mazingira ya Shuleni yanakuwa yenye kuvutia lakini ubinifu katika ufundishaji wa Masomo ili kuhakikisha wanafunzi katika Shule zenu wanafanya vizuri"amesema Mageni

Mwalimu Mageni pia amewataka uongozi wa Shule kwa maana ya Mkuu wa Shule, Mwalimu Mkuu msaidizi pamoja na Mtaaluma kuhakikisha wanawajali walimu na watumishi wengine waliopo katika shule zao, kwakufanya hivyo kila mmoja atajituma katika kutekekeleza majukumu yake jambo litakalosaidia kuongeza ufaulu wa wanafunzi wao.

Aidha Mwalimu Mageni ameongeza kuwa kila Shule kupata ufaulu asilimia mia inawezekana endapo kila mwalimu atasimama katika nafasi yake na kujituma ikiwa ni pamoja na walimu wakuu kuwajua walimu wao na masomo yao wanayofundisha lakini pia kujiwekea malengo na kuhakikisha yanatimia
.

# TURUDI KWENYE MISINGI YETU YA KUDUMISHA AMANI



Mkuu wa wilaya ya chunya Mhe, Mbarak Alhaji Batenga aliwataka wananchi wa Chunya kuendelea kuliombea Taifa la Tanzania na Viongozi wake ili Amani iliyopo iendelee kudumu huku akiwasisitiza wananchi wote bila kujali dini na dhehebu Kulinda na kudumisha Amani jambo liotakalofanya tuendelee kujihusisha na shughuli za maendeleo na Jambo hilo linawezekana kwa njia ya Maombi. Kauli hiyo aliitoa tarehe 22.Aprili 2024 wakati wa dua na Maombi ya kuliombea Taifa katika maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano wa Tanzania yaliyofanyika katika Ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya (Sapanjo).

"'Ili Amani iweze kupatikana lazima watu wakubali kutenda haki tusipotenda haki tunatafuta kuvuruga amani kama wewe ni mtumishi tenda haki katika nafasi yako ,ukiwa wewe ni mfanyabiashara tenda haki katika afasi hiyo ,tunapokuja kuliombea Taifa nasisi pia tujiombee kwasababu kama amani inavurugika sisi ndio tunaovuruga."alisema Batenga

Mwenyekiti jumuiya ya maridhiana ya Amani Wilaya ya Chunya Mch Anyandwile Kajange kutoka kanisa la Moraviani kwa niaba ya viongozi wa Dini zote alimpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan kwa miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa wilayani Chunya pamoja na kuendelea kuilinda na kuidumisha Amani huku akiomba Serikali kuingilia kati Matumizi ya Mitandao ili kudhibiti mmomonyoko wa Maadili kwa Taifa.

Nao viongozi wa dini sheikh Abdulijalili Jambia na Fr Kanon Mapunda Mchungaji kutoka Kanisa la Angikana kwaniaba ya Viongozi wa dini wamewaongoza wananchi wa wilaya ya Chunya katika dua na maombi ya kuliombea Taifa la Tanzania pamoja na viongozi wote ili kuendelea kudumisha amani na kuulinda Muungano pamoja na kuomba Mungu aliepushe Taifa dhidi ya majanga mbalimbali.

Awali akitoa salama Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya Ndugu Tamimu Kambona amewapongeza wananchi wa Chunya kwa utulivu, ushiriki wao kwenye miradi ya maendeleo na kuwataka kwendelea kuilinda Amani iliyopo pamoja na kudumisha Muungano wa Tanzania.

"Niwashukuru Mkuu wa Wilaya,Viongozi wa Chama, viongozi wa dini mbalimbali ,waheshimiwa madiwani na wananchi kwa Ushirikino mkubwa mnaotupatia kama Halmashauri, niwaombe ushirikiano huu mwendelee kuutoa lakini pia twendelea kuimarisha Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar kwani Muungano huu tulinao ndio unaotufanya twendelee kuishi kwa Amani bila ubaguzi wa aina yeyote."alisema Kambona.

Ibada hiyo ya Dua na Maombi ya kuliombea Taifa ilifanyika leo, katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya (Sapanjo) ikiwa ni kuelekea Maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano wa Tanzania, Ibada imehudhuriwa na viongozi mbalimbali wa dini, Viongozi wa Chama cha Mapinduzi CCM, Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya , Wanafunzi pamoja na wananchi wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya.





## MKIPATA FURSA NYINGINE KAMA HIZI KARIBU SANA CHUNYA

Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauru ya wilaya ya Chunya Ndugu Tamim Kambona amewaomba shirika la Hellen Keller Internation na shirika la Himalayan Cataract Project (HCP) na wadau wote kuendelea kuja Chunya ili kuwahudumia wananchi wa wilaya ya Chunya jambo ambalo litaendelea kuimarisha afya za wananchi wa Chunya na hata wananchi kutoka nje ya wilaya ya Chunya kwakufanya hivyo uchumi wa wananchi wa Chunya na Tanzania kwa ujumla utaendelea kuongezeka

Ametoa rai hiyo tarehe 24/6/2024 wakati alipowatembelea wanufaika wa huduma ya Uchunguzi na upasuaji wa Mtoto wa Jicho, pamoja na Madaktari bingwa wa Macho wanaoendelea kutoa huduma za matibabu ya ugonjwa wa Macho (Mtoto wa Jicho) katika Hospitali ya wilaya ya Chunya, huduma iliyodumu kuanzia tarehe 19/6/2024 mpaka tarehe 24/06/2026

“Hili jambo linalofanyika kwa wilaya ya Chunya halijawahi fanyika hapo awali na limejumuisha wananchi wengi wenye matatizo ya macho wilayani Chunya na Nje ya wilaya ya Chunya huku wengine wakisafirishwa kwa zaidi ya kilometa 200 na wameendelea kupata matibabu. Lakini tumeshuhudia watu walikuwa hawawezi kuona kwa zaidi ya miaka mitatu, minne na wengine saba lakini sasa wanaona. Na wengine wameshuhudia hapa kwamba wamehangaika maeneo mengi bila mafanikio lakini kupitia hiki kinachofanyika hapa watu wamepata suluhu”. Alisema Ndugu Kambona

Aidha Ndugu Kambona amewashukuru shirika la Hellen Keller Internation na shirika la Himalayan Cataract Project (HCP) kuendelea kutoa uelewa na ufahamu zaidi kwa watalamu wa ndani kwani nao walikuwa wanahusika



kwa namna moja au nyingine kwenye uchunguzi na upa-



suaji wa mtoto wa Jicho ili kujipatia uzoefu wananchi wa Chunaya waendelea kupata matibabu kupitia utaalamu na uzoefu walioupata, Huku Hellen Keller Internation na shirika la Himalayan Cataract Project (HCP) watakapopata nafasi tena tunawakaribishwa kuja Chunya kutoa huduma kama hizi, Kwa niaba ya wananchi wote wa Chunya Tunawashukuru sana

Meneja wa mradi wa matibabu ya Macho Ndugu Athuman Tawaqal alitoa wito kwa mashirika mengine kuendelea kushirikiana na Serikali ili kutatua changamoto za wananchi wa Tanzania jambo ambalo litasaidia kuleta furaha kwa wananchi ambao wamekuwa na changamoto nyingi lakini wameshindwa kuzipatia suluhu wao wenyewe na ameongeza kuwa changamoto ni kubwa sana hivyo nguvu zaidi inatakiwa.

Kiongozi wa Jopo la Madaktari Bingwa Daktari Barnabas Mshangila alisema lengo lilikuwa kuwahudumia wananchi 450 wenye matatizo ya macho (Mtoto wa Jicho) lakini mpaka muda huu ikiwa ni siku ya mwisho tumesha hudumia wagongwa mia nne na ishirini hivyo ni matumaini yao lengo litafikiwa. Dkt Mshangila ameongeza kuwa huduma hii huleta furaha kwa watu wengi hasa pale ambapo mgonjwa alikuwa hajawai kuona na sasa kupitia huduma zilizotolewa zimemsaidia kuona tena hivyo lengo la kuleta matibabu linakuwa limefikiwa vizuri na limerudisha furaha kwa wananchi wa wilaya ya Chunya na hata watanzania kwa ujumla wake



"Tulimopokea binti mwenye mume na watoto wawili lakini kutokana na changamoto ya mtoto wa jicho alikuwa hajawahi kuwaona watoto wake na hata mumewe hivyo kupitia huduma hii ameweza kuwaona watoto wake pamoja na mumewe hivyo alipata furaha" alisema Daktari Mshangila

Kambi ya Matibabu ya Macho ilianza rasmi tarehe 19/06/2024 na kuhitmishwa tarehe 24/06/2024 zoezi hilo lilihitimishwa kwa kuwapatia huduma ya upasuaji jumla ya wagonjwa 481, Ikumbukwe huduma za uchunguzi na upasuaji zimetolewa bure kabisaa bila kujali umri, umbali na vigezo vingine vyovyote.

# SERIKALI ITAENDELEA KUPOKEA MAELEKEZO YA CHAMA KATIKA KUTATUA CHANGAMOTO ZA WANANCHI




Mkuu wa wilaya ya Chunya Mhe Mbarak Alhaji Batenga alisema Serikali wilaya ya Chunya itaendelea kupokea maelekezo ya Chama na kuyatekeleza pamoja na kuhakikisha yale yaliyoahidiwa kwenye Ilani ya Uchaguzi yanatekelezwa kwa asilimia mia moja ili kuondoa maswali kwa wananchi wa Chunya kuhoji uhitaji au ubovu wa miundombinu yoyote ile ya utoaji wa huduma.

Ametoa kauli hiyo tarehe 30/5/2024 wakati akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Igundu kwenye viwanja vya Shule ya Msingi Igundu wakati wa Hafla ya kukabidhiwa mradi wa Maji uliotekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia RUWASA, Shirika na Catholic Relief Services (CRS) pamoja na wananchi wa Igundu

“Sisi kama Serikali tunaahidi kuendelea kupokea maelekezo ya Chama na kuyatekeleza ili kuondoa Maswali kutoka kwa wananchi kuhusu Serikali yao, Wananchi waendelee kuiamini Serikali yao kwani ni sikivu na yenye kuwajali wananchi wake” Alisema Mhe Batenga

Diwani wa kata ya Sangambi Mhe Junjuu Muhewa kwa niaba ya wananchi wa Kijiji cha Igundu na Kata ya Sangambi kwa ujumla aliwashukuru Shirika na Catholic Relief Services (CRS) pamoja na Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kupelekewa fedha nyingi za kutekeleza miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na mradi wa maji uliokabidhiwa kwa wananchi wa Igundu baada ya kukamilika kwa asilimia mia moja

“Nimehemewa na furaha kwasababu ya furaha, Naomba nitoes Shukrani zangu kwa Shirika hili la CRS linalofanya kazi kwa karibu na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan. Pamoja na Mradi huu wa Maji tunaokabidhiwa leo kata yangu ya Sangambi imepokea fedha zaidi ya Bilioni Mbili kutekeleza miradi mbalimbali hivyo naomba nipelekee salamu zangu na za wananchi hawa wa Igundu na wananchi wa kata ya Sangambi kwa Mhe Rais Samia kwamba

wanasangambi tunamshukuru sana" Alisema Mhe Junjulu Meneja wa RUWASA wilaya ya Chunya Mhandisi Olineno Sanga amesema utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwenye sekta ya Maji wilaya ya Chunya imefikia asilimia themanini na tano (85%) huku akisema mipango yao ifikapo 2025 kata ya Sangambi itafikia asilimia mia moja katika upatikanaji wa Maji safi na salama kwa matumizi ya Binadamu "Kwa maana ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi tumeshafikia azma ya Serikali kwa maana ya asilimia themanini na tano (85%) lakini pia tumekuwa na mipango mbalimbali tumebakiza kijiji kimoja cha Shoga lakini pia kitongoji kimoja cha Dendeluka, Rais ameshatoa fedha kwaajili ya upatikanaji wa Maji kwenye maeneo hayo na ni matumaini yetu ifikapo 2025 tutafikia asilimia mia moja upatikanaji wa maji katika kata ya Sangambi" Amesema Mhandisi Sanga

Mkuu wa ofisi ya CRS Mkoa wa Mbeya Bi Marilyn Chottah alisema, Mradi huo umegharimu shilingi milioni mia nne thelasini na nne huku asilimia zaidi ya themanini ya fedha hizo zikitolewa na shirika la CRS na mradi unalenga kuwahudumia wananchi 4883 wa Kijiji cha Igundu huku Taasisi za Serikali kama vile Zahanati ya Igundu na Shule ya Msingi ya Igundu zikinufaika moja kwa moja na mradi huo kwa kujengewe miundombinu mbalimbali ya maji ambayo imeunganishwa moja kwa moja na maji hayo



"Mradi huu umegharimu shilingi milioni mia nne thelasini na nne elfu mia mbili sabini na tano na laki tatu na hamsini na sita elfu (434,275,356,000/=) huku shilingi milioni mia tatu sabini na tano ambazo ni sawa na silimia 86.5% ya fedha zote za mradi zikitolewa na shirika na Catholic Relief Services (CRS) na Lengo na Mradi ni kuwahudumia wananchi wa Igundu ili waepukane na changamoto ya maji" Alisema Bi Chottah Shirika na Catholic Relief Services (CRS) linatekeleza miradi mbalimbali katika Halmashauri ya wilaya ya Chunya huku Mradi wa Ifumbo umeshakamilika na unatumika, Mradi wa Igundu kata ya Sangambi umekamilika na umekabidhiwa Jana tarehe 30/5/2024 na Mradi mwingine unatekelezwa kata ya Kasanga kijiji cha Soweto umefikia asilimia karibu Themanini (80%) na Lengo kubwa ya CRS ni kuhakikisha linashirikiana na Serikali kutatua changamoto za wananchi wa wilaya ya Chunya zinatatuliwa kwa wakati.





## HAKUNA MALIPO YOYOTE YATAKAYOPITISHWA BILA KULIPA DENI RUWASA

Katibu tawala wa wilaya ya Chunya ndugu Anakleth Michombero amezitaka taasisi zote za Serikali zinazodaiwa na RUWASA wilayani Chunya kulipa mara moja madeni yao huku akisema hakuna malipo yoyote yatakayofanyika kwa taasisi zote ambazo ziko chini ya Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya mpaka watakapokuwa wamelipa madeni yao kwa Mamlaka ya maji safi na usafi wa mazingira RUWASA.

Akizungumza tarehe 25/05/2025 kwenye ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya (Sapanjo) wakati akimwakilisha Mkuu wa wilaya ya Chunya kufungua mafunzo ya kuwajengea uwezo vyomba vya utoaji maji (CBWSO) vilivyopo ndani ya Halmashauri ya wilaya ya Chunya lengo likiwa ni kuhakikisha vyombo hivyo vinajiendesha

"Naomba kutoa maelekezo ambayo Mkuu wa wilaya ameniagiza, Taasisi zote zenye madeni mfano Shule ya Msingi Mapogolo pamoja na Zahanati ya Mapogolo kuhakikisha wanalipa madeni yote, na hili tunaanza sasa hivi kulishughulikia maana taasisi hizo zote ziko chini ya Mkurugenzi hivyo hakuna malipo yoyote yatafanyika mpaka tuone taasisi hizo zimelipa madeni yao kwa RUWASA". Amesema Michombero

Aidha aliwataka viongozi wa Serikali na wadau wengine kutambua mipaka yao ya utendaji kazi jambo ambalo litasaidia kuepusha mwingiliano na migongano ya majukumu kwa viongozi wa Vyombo na viongozi wengine katika eneo husika na kwakufanya hivyo itasaidia vyombo hivyo kuongeza upana wa matumizi ya maji kwa wananchi wa maeneo husika

"Niwaombe sana kila mmoja atambue majukumu yake, wakati mwingine kuheshimu mamlaka moja haikufanyi wewe kuondolewa nafasi yako, Mfano mimi ni mjumbe kwenye kamati mbalimbali na nikiwa katika vikao hivyo natambua muda wa kuwa mjumbe na natambua muda wa kuwa DAS, Hivyo niwaombe viongozi wenzangu kila mmoja atambue mipaka ya majukumu yake" Aliongeza Michombero

Mwakilishi wa meneja wa RUWASA Mkoa wa Mbeya Mhandisi Erasto Vincent Saronga alisema mafanikio makubwa yaliyopo ndani ya RUWASA Chunya yanachagizwa na ushirikiano mzuri uliopo kati ya uongozi wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya na uongozi wa RUWASA Chunya, na ameomba ushirkiano huo uendelee ili kwa pamoja waweze kufikia malengo yaliyokusudiwa

Naye kaimu meneja wa RUWASA wilaya ya Chunya Mhandisi Olineno Sanga amesema lengo la RUWASA kuwajengea uwezo viongozi wa vyombo wa watumia maji



ni kuhakikisha wanasimamia vizuri makusanyo ya fedha za maji kwenye miradi yao na kuwaongoza katika matumizi bora ya fedha hizo na hatimaye waweze kutatua changamoto za mradi wa maji kwa wakati na kwa uwazi ili wananchi waweze kupata taarifa zote kuhusu miradi ya maji iliyo katika maeneo yao wanayoishi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya Mhe Bosco Mwanginde aliwataka washiriki wote kufuatilia vizuri maelekezo hayo huku akiwahakikishia Madiwani waliopo kwenye maeneo ya miradi ya maji yanayosimamiwa na wananchi kupitia vyombo vya watumia maji kwamba wanapowafuatilia kwa kuhoji maswali lengo lao ni kuona wananchi wanapata maji hivyo wakati mwingine wanaweza kuwauliza viongozi wa vyombo vya watumia maji ili kujiridhisha na mwenendno wa utoaji wa maji kwa wananchi wake.

Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya ndugu Tamim Kambona amewataka viongozi wa watumia maji Chunya kuhakikisha wanasimamia vizuri makusanyo ya fedha ili kuweza kuhudumia miundombinu ya maji katika maeneo yao huku akiwataka kutochanganya fedha za maji na fedha nyingine za makusanyo yanayofanyika kwenye vijiji kwani Vyombo vya wasimamia maji ni taasisi inayojisimamia.

Mafunzo hayo yalofanyika 25/5/2024 katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya (Sapanjo) yakihudhuriwa na Viongozi wa Vyombo kutoka kwenye maeneo husika, madiwani kutoka kwenye maeneo ya miradi husika, watendaji wa kata pamoja na maafisa wa RUWASA kutoka Mbeya na lengo likiwa ni kuwajengea uwezo viongozi hao katika kusimamia miradi ya maji iliyopo katika maeneo yao.



# SUALA LA LISHE HUANZIA TUMBONI KWA MAMA



Mkuu wa wilaya ya Chunya Mhe Mbarak Alhaji Batenga amewataka wakina baba wote wilayani Chunya kuhakikisha wanawasaidia wake zao na wakina mama wengine waliopo katika maeneo yao kupata lishe bora kabla ya kubeba ujauzito, wakati wa ujauzito na hata baada ya kujifungua kwani suala la lishe kwa mtoto huanzia Tumboni kwa mama yake

Akizungumza kwenye maadhimisho ya Afya na lishe kwa ngazi ya kijiji yaliyofanyika tarehe 18/6/2024 katika kijiji cha Ifumbo kilicho katika kata ya Ifumbo, ikiwa ni mwendelezo wa maadhimisho hayo ambapo wilaya ya Chunya hufanya kila robo ya mwaka lengo ikiwa ni kuhimiza Afya bora na Lishe bora kwa mtoto na jamii kwa jamii kwa ujumla Mhe Batenga amesema wakina baba (wanaume) watambue kuwa hilo nalo ni jukumu lao

“Tukaboreshe lishe, hivi vitu (Vyakula katika Makundi mbalimbali ya Lishe) havitoki Mbinguni na vingine tukapande wenyewe ili tuwapatie lishe bora familia zetu. Wakinababa tuwasaidie wakinama ili wapate lishe bora maana suala la lishe linaanza tumboni na kwakufanya hivyo tutakuwa tumetekeleza vyema suala la kujali familia zetu” alisema Mhe Batenga

Akitoa taarifa ya hali ya Lishe wilaya ya Chunya, Mganga Mkuu wa wilaya ya Chunya Dkt Darison Andrew amesema wanaume wengi hawawajibiki ipasavyo katika kuhakikisha mama wajawazito wanapata lishe bora na sababu ni kukosekana kwa Elimu ya Lishe, Hivyo ni tamaa yao kuona wanaume wakiambatana na wenza wao wanapokuja kliniki ili waweze kupata Elimu hiyo muhimu

“Ni tamaa yetu kuona wanaume wengi wanapata elimu hii sababu mtoto aliyedumaa hana mchango mkubwa sana



katika maendeleo ya Taifa na hata akisoma uelewa wake utakuwa mgumu sana, hivyo ni tamaa yetu mama mjamzito apate vyakula vyote kama vilivyowekwa kwenye meza ile na mtoto atakapotimiza miezi saba baada ya kuzaliwa akipata lishe bora itamjenga katika maisha yake yote"

Aidha, Dkt Darison Andrew ameongeza kuwa katika wajawazito 100, wajawazito 2 mpaka 9 wanakuwa na upungufu wa damu mwilini hivyo anakuwa na upungufu wa kinga mwili jambo ambalo linamuweka hatarini kupoteza maisha wakati wa kujifungua.

itasaidia kupata Taifa lenye watu wenye afya bora

Kwa niaba ya wananchi wa kata ya Ifumbo waliojitokeza kwenye maadhimisho hayo ya Afya na Lishe, Diwani wa kata ya Ifumbo Mhe. Weston Mpyila amesema suala la Lishe katika kata ya Ifumbo ni la lazima na wananchi wa Ifumbo wanazingatia hilo kwani mpaka sasa watoto wanapata Lishe wawapo nyumbani na hata wakiwa shuleni kwani vyakula vipo.

"Tunafanya jitihada kuhakikisha watoto wetu wanazingatia suala la lishe, sisi suala la lishe ni lazima sio ombi tena na kilimo tunafanya vizuri kwani vyakula vyote ulivyoona hapa mbele tunalima wenyewe hivyo sisi lishe sio tatizo" Alisema Mhe Mpyila

Muhudumu wa Afya ngazi ya kata bwana Charles Jailos Ngazi amesema Elimu hii ya lishe huwa inatolewa mara kwa mara kwenye zahanati na vituo vyao vya afya huku akisema elimu hiyo imepokelewa vizuri na wananchi, kwani mwitio wao ni mkubwa huku akirejerea idadi kubwa ya wananchi waliojitokeza katika siku ya Afya na lishe.



Siku ya Afya na Lishe huadhimishwa na kila kijiji kwa kila Robo ya mwaka huku uongozi wa Halmashauri kwa kuongozwa na maafisa lishe wa wilaya ya Chunya huchagua kuhudhuria katika maadhimisho ya kijiji kimojawapo ili kuongeza chachu ya kuthamini lishe pamoja na kutoa elimu zaidi kuhusu lishe, kwa Robo hii ya nne uongozi ulitembelea siku ya afya na lishe katika kijiji cha Ifumbo ndani ya kata ya Ifumbo.

Amewaomba wananchi wa Ifumbo na Chunya kwa ujumla kuwapatia lishe bora wajawazito na kwakufanya hivyo wananchi wameitikia, kwani chakula kinatolewa katika Taasisi zote za shule za binafsi na Serikali, lakini pia kwenye



## MHE BATENGA; RAIS ANAZIJUA CHANGAMOTO ZINAZOWAKABILI WANACHUNYA NA ANAZITATUA ZOTE

Mkuu wa wilaya ya Chunya Mhe Mbaraka Alhaji Batenga aliwahakikishia wananchi wa wilaya ya Chunya kwamba Mhe Rais Samia Suluhu Hassan anatambua changamoto zote zinazowakumba wananchi wa Chunya na anazipatia majibu changamoto moja baada ya nyingine huku akirejerea Ujenzi wa Kituo cha Afya Kambikatoto, Ujenzi wa Shule ya Sekondari na sasa Utekelezaji wa mradi wa Maji unaotaraji kuanza hivi karibuni.

Akizungumza na wananchi wa kata ya Kambikatoto tarehe 29/5/2024 baada ya kumkabidhi mkataba wa utekelezaji wa mradi huo mhandisi Richard Juma kutoka Kampuni ya Equiplus Company Limited inayotaraji kutekeleza mradi huo Mhe Batenga aliwataka wananchi kuwa na Imani na Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan kwani changamoto zote zinapatiwa Suluhu kwa wakati "Kurahisisha upatikanaji wa Matibabu ya Kibingwa Mhe Rais ametuletea madaktari Bingwa hapa hapa wilayani Chunya, Kituo cha Afya kimejengwa hapa Kambikatoto, Sekondari imejengwa hapa na wanafunzi tayari wanasoma hapa ndugu wananchi Mhe Rais Hajawafikia? Niwaombe muendelee kuiamini Serikali hii ya awamu ya sita na ndo maana leo mradi wa maji unaanza kutekelezwa hapa kwenu" Alisema Mhe Batenga Awali akitoa taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maji katika Halmashauri ya wilaya ya Chunya Meneja wa RUWASA



wilaya ya Chunya Mhandisi Olineno Sanga alisema Halmashauri ya wilaya ya Chunya imepokea fedha zaidi ya Bilioni tano ili kutekeleza miradi mbalimbali ya maji ndani ya wilaya ya Chunya huku akisema miradi mingine imekamilika na mingine iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.
"Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Halmashauri ya wilaya ya Chunya tumepokea fedha bilioni tano na milioni mia tisa ambapo bilioni nne zimepelekwa kwenye mradi wa Maji wa Matwiga wakati pesa zinazobaki zimepelekwa kwenye miradi mbalimbali ikiwepo uchimbaji wa visima katika vijiji kwa Bitimanyanga, Mafyeko, Mtanila, Lupa na Mamba na miradi ya Uchimbaji wa visima inatakiwa kuisha tarehe 30 juni" Alisema Mhandisi Sanga
Mhandisi kutoka Kampuni ya Equiplus Company Limited Mhandisi Richard Juma kwa niaba ya Kampuni yake amesema wamejipanga kutekeleza mradi huo kwa ubora, ufanisi na mradi utatekelezwa ndani ya muda uliopangwa huku akiishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuiamini Kampuni hiyo katika kutekeleza mradi huo.
Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya Mhe Bosco Mwanginde amewashukuru sana wananchi wa kata ya Kambikatoto kwa namna wanavyoshiriki katika ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwenye maeneo yao huku akiwataka kufanya hivyo pia kwenye mradi maji unaotaraji kuanza kutekelezwa katika kata yao ya Kambikatoto.
Mradi wa Maji unaotaraji kutekelezwa katika kata ya Kambikatoto utagharimu fedha shilingi milioni mia tano tisini na tano, unajengwa na Kampuni inayoitwa Equiplus Company Limited ambapo utajengwa kwa miezi sita hivyo mradi huo utakamilika mwezi Disemba na utakapokamilika utahudumia wananchi wa kijiji cha Kambikatoto kwa asilimia mia moja



# Michezo

**UJENZI WA UWANJA WA MICHEZO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA UTAONGEZA UCHUMI WA WANANCHI WA CHUNYA**

Timu ya KENGOLD ya Chunya Mkoani Mbeya iliyoibuka na ushindi wa ligi daraja la kwanza na kufanikiwa kutwaa kombe la NBC Championship huku ikifanikiwa kupanda Ligi Kuu msimu ujao wa soka 2024/2025 imeongeza hamasa kubwa katika Ujenzi wa Uwanja wa Michezo wa Wilaya ya Chunya uliopo kata ya Mbugani .



Viongozi wa Wilaya wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Chunya Mhe Mbarak Alhaji Batenga, Madiwani wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya wakiongozwa na Mwenyeki wa Halmashauri, Ofisi ya Mbunge wa Jimbo la Lupa, Ofisi ya Mkurugenzi, Wadau wa Soka na Wadau wa Maendeleo wamekuwa na msukumo mkubwa wa kuhakikisha Uwanja huo unakamilika na kuanza kutumika ili kuziwezesha ligi mbalimbali za Wilaya, Mkoa na Timu za kitaifa kucheza katika Uwanja huo

Hamasa hiyo imekuja kupitia ombi la Timu ya mpira wa miguu ya KENGOLD lililotolewa tarehe 09/05/2024 mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Chunya alipo mwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mbeya wakati wa hafla ya Mapokezi ya Timu ya Mpira wa Miguu ya KENGOLD iliyorudi nyumbani na Ushindi, Hafla iliyofanyika katika uwanja wa Mpira wa miguu Sinjilili Halmashauri ya Wilaya ya Chunya.

“Ombi lenu la kukamilika kwa uwanja nimelipokea na linafanyiwa kazi na niwaahidi uwanja wetu utakamilika , tunataka mashindano mbalimbali yafanyike katika viwanja vyetu, timu ya Simba na Yanga zije zicheze katika viwanja vyetu pamoja na mashindano mengine yakayokuwa yanafanyika katika ngazi mbalimbali“.alisema Mhe. Batenga.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya Mhe. Bosco mwanginde naye akawataka wadau mbalimbali wa maendeleo kujitokeza kuchangia ujenzi wa uwanja unaojengwa katika kata ya mbugani ili timu mbalimbali ziweze kufika na kucheza katika uwanja huo kwani faida ya timu zinapokuja kucheza ni biashara lakini pia burudani kwasababu wafanyabiashara watapata fursa ya kuuza bidhaa zao na kutoa huduma mbalimbali na hatimaye kujipatia kipato.

“Chunya kama itakuja timu ya Simba au Yanga tunajua tuna uhakika wa kufanya biashara kwani timu ni biashara na burudani kwahiyo nawaombeni sana wadau mliopo hapa tuchange michango yetu ili tukamilishe uwanja wetu kusudi timu mbalimbali ziweze kuja kucheza Chunya, mimi na Mkurugenzi wangu tayari tumetenga bajeti na tutasimamia kuhakikisha fedha zilizotengwa zinafanya kazi hiyo” alisema Mhe. Mwanginde.

Mara baada ya Hafla ya mapokezi ya Timu ya KENGOLD mikakati mbalimbali imeendelea kufanyika kwaajili ya kuhakikisha Uwanja wa michezo wa Wilaya unakamilika ikiwa ni pamoja na kufanya harambee ya kuchangia Ujenzi huo ambao ulihusisha wadau mbalimbali wa maendeleo na Wadau wa Soka, kwani Mkuu wa Wilaya ya Chunya Mhe. Mbarak Alhaji Batenga amekuwa na Imani na wadau hao kwakua wamekuwa wakijitoa sana kwa hali na mali katika Sekta mbalimbali ikiwemo Michezo ambapo wadau hao walianza kushiriki ujenzi wa uwanja huo tangu mwaka 2013.

“Mimi nina Imani sana na wadau hawa hawajawahi kutuangusha katika shughuli mbalimbali za Maendeleo katika Wilaya yetu

, tunatamani ifikapo mwezi wa nane Uwanja uwe umekamilika ili timu ziweze kuja kucheza Chunya kwani tunataka kuileta Tanzania Chunya na Chunya tuipeleke Tanzania" alisema Mhe. Batenga.
Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Mhe. Juma Zuberi Homera ambaye alikuwa mgeni rasmi wakati wa hafla ya Harambee ya kuchangia ujenzi wa uwanja wa Michezo wa Halmashauri ya wilaya ya Chunya amesema kuwa kuna faida nyingi timu zinapokuja kushiriki ligi katika viwanja vya Chunya kwani wafanyabiashara mbalimbali wa hotel , Mamalishe na wasafirishaji itakuwa ni fursa kwao kufanya biashara na kujipatia kipato kwaajili ya kukuza uchumi wao pamoja na Halmashauri kujipatia mapato na hatimaye kukuza uchumi wa Chunya
"Uwepo wa timu kushiriki ligi kuu hapa watu wenye magari mtafanya biashara sana, watu wenye Hotel watu watalala hapa, Hotel zote zitajaaa lakini pia mama lishe nao watafanya biashara kwani kunapokuwa na mechi watu wengi sana wanasafiri na timu jambo ambalo litapelekea kukuza uchumi wa Chunya na Halmashauri itajipatia mapato Chunya"alisema Mhe. Homera.
Akitoa Salama katika harambee ya kuchangia Ujenzi wa Uwanja wa Michezo Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi ndugu Noel Chiwanga ametoa rai kwa wadau kwendelea kuwa wazalendo kwa kumuunga Mkono Mkurugenzi wa Timu ya Kengold ndugu Keneth Mwakyusa ili kuendeleza Michezo katika Wilaya ya Chunya kwani kwa kufanya hivyo italeta hamasa kwa wadau wengine kuunga Mkono sekta ya Michezo.
Naye Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ndugu Athumani Bamba amewashukuru Wadau kwa kuendelea kushirikiana na Halmashauri katika shughuli mbalimbali za maendelao na kuwaomba kuunga mkono jambo la Ujenzi wa Uwanja wa Michezo ili uwanja uweze kukamilika na kutumika kwaajili ya michezo mbalimbali.
Katika Harambee hiyo ya kuchangia Ujenzi wa Uwanja wa Michezo Wilaya ya Chunya iliyoongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Mhe. Juma Zuberi Homera michango mbalimbali imeweza kutolewa na wadau ikiwa ni pamoja na Mifuko ya Saruji 400, Mchanga Lori 10, fedha taslimu Millioni 3,240,000/= ahadi milioni 61,669,000/= pamoja na Kokoto zenye thamani ya Tsh 10,000,000/=.



# Neo la Mhariri Mkuu

"Hatupoi Hatuboi) katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, kwani miradi ya maendeleo inayotekelezwa wilayani Chunya inafanyika kwa viwango na weledi Mkubwa sana Mfano upanuzi wa Hospitali ya wilaya, ujenzi wa miradi ya Madarasa na miradi mingine mingi
Wilaya ya Chunya inajenga uwanja wa michezo na kazi inaendelea, uwanja ule ukikamilika kwanza tutakuwa Halmashauri ya kwanza kumiliki uwanja wa Michezo lakini Halmashauri itajipatia mapato kutokana na shughuli mbalimbali zitakazokuwa zinafanyika katika uwanaja huo lakini wananchi mbalimbali watajipatia fursa mbalimbali kulingana na mwingiliano wa watu utakaosababishwa na uwepo wa uwanja huo
Pia Halmashauri inajenga stendi kubwa, nzuri nay a kisasa ili kuendana na maendeleo yanayofanyika kwenye wilaya ya Chunya, kwasasa wilaya ya Chunya inapokea mabasi mengi na kati ya mabasi hayo tayari tuna kampuni mbili zinapeleka mabasi yao nje ya mkoa wa Mbeya hivyo tunajenga stendi ili kuweza kuendana na hadhi hiyo.
Dhana ya "Chunya Hatupoi Hatuboi" ina ukweli wa wazi kabisa Chunya, Pamoja na Mambo makubwa yanayofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Halmashauri yetu, Hivi karibuni tunataraji kujenga kituo cha Redio lengo letu ni moja tu kuhakikisha wananchi wanapata habari za maendeleo yao kwa uwazi Zaidi
Mwisho sio kwa Umuhimu, Wananchi wa wilaya hii ya Chunya niwaombe muendelee kuiamini Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan, Ninyi na mashuhuda wa kazi kubwa inayofanywa katika maeneo yenu, Sisi kazi yetu ni kusimamia tu. Niwaahidi wanachunya kwamba Mambo mazuri yanakuja

# HABARI PICHA



*Halmashauri ya wilaya ya Chunya imeshiriki kwa kishindo Maadhimisho ya siku ya wafanyakazi maarufu kama Mei Mosi ambayo huadhimishwa kila tarehe moja ya mwezi wa tano ya kila mwaka, kwa mwaka 2024 maadhimisho hayo Mkoa wa Mbeya yamefanyika katika Halmashauri ya wilaya ya Rungwe katika viwanja vya Chuo cha Ualimu Mpuguso ambapo Halmashauri ya wilaya ya Chunya iliwakilishwa na zaidi ya watumishi 80.*




*Halmashauru ya wilaya ya Chunya iliungana na wananchi wa Taifa la Tanzania pamoja na Mataifa Mengine Duniani kuadhimisha siku ya Familia ambapo Halmashauri ya wilaya ya Chunya ilifanya Maadhimisho hayo tarehe 15/5/2024 katika Ukumbi wa Mikutano wa Roman Catholic uliopo katika kata ya Lupa, ambapo wazazi na walezi wakikutanishwa na maafisa kutoka Halmashauri na asasi zisizo za kiserikali ili kujadili hatma njema ya Taifa la Kesho kwa kumjali mtoto kwanza*




*Mkuu wa wilaya ya Chunya Mhe Mbaraka Alhaji Batenga ameongoza kamati ya Usalama ya wilaya ya Chunya ikiambatana na watalaam kutoka Halmashauri ya wilaya ya Chunya kukagua miradi itakayopitiwa na Mwenge wa Uhuru mwaka 2024 utakapokimbizwa katika Halmashauri ya wilaya ya Chunya mapema mwezi August. Ziara hiyo ilifanyika tarehe 12/06/2024*
*Mwenge wa Uhuru utakupokelewa tarehe 24/08/2024 katika kijiji cha Bitimanyanga kilichopo kata ya Mafyeko ukitokea Mkoani Tabora na baadaye kukimbizwa katika Halmashauri ya wilaya ya Chunya ambapo utakagua miradi mbalimbali katika Nyanja za Elimu, Afya, Maji, Barabara na Miradi mingine mingi.*



*Afisa Elimu Mkoa wa Mbeya Mwalimu Kiduma Mageni, Akizungumza jambo wakati wa Mahafari ya Kidato cha Sita katika Shule ya Sekondari Kiwanja*

# CHUNYA

## JARIDA LA MTANDAONI



## HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA

S.L.P 73 CHUNYA, MBEYA
SIMU: 025 2520121

www.chunyadc.go.tz
chunyadc_official
@ chunya_official
ded@chunyadc.go.tz

*Imetolewa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini*